

# Umbali Kati ya Mtu na Mwingine ina Maanisha nini?

Umbali kati ya mtu na mwingine ina maanisha kuweka umbali wa mwili kati ya mtu mmoja na watu wengine. Kufanya hivi ina saidia kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa. Wakati wa mlipuko wa ugonjwa huu ni lazima KILA MTU afanye wajibu wake kupunguza virusi vya COVID-19.

## Umbali kati ya mtu na mwingine unasaidiaje?



Unasaidia kuvunja mnyororo wa kuenea.

Unasaidia kupunguza hatari ya kuwa karibu na mtu aliyeambukizwa au eneo lililoambukizwa.

## Je, ni jinsi gani unaweza fanya wajibu wako?



Kaa nyumbani.

Inafaa kufuta mikusanyiko nje ya nyumba au ya watu zaidi ya 10.

Ni lazima kila mtu na familia yake wakae nyumbani.

## Je, ninaweza kutembelea wazazi wangu au familia yangu?



Wazee wanakadiriwa kuwa hatarini zaidi, kwa hiyo, kama kuwatembelea siyo muhimu – kama vile kwenda kuwasaidia, basi ieleweke kwamba kutokugusana nao kunawaweka wao salama Zaidi kutoka virusi ya COVID-19.

## Je, marafiki zangu wa karibu wanaweza kunitembelea?



La, usiwe na marafiki kwa nyumba na usiende popote. Jaribu kuzuia ziara za kijamii kwa sasa.

Bado ni muhimu kuwasiliana na wapendwa kwa wakati huu. Jaribu kutumia njia zingine kama simu za video kuongea na marafiki.

## Je, watoto wanaweza kulala au kucheza kwa marafiki zao?



Watoto hawawezi kucheza au kulala na watoto wengine. Watoto wote wanaweza kucheza nje, lakini ni lazima watoto wabaki umbali wa futi sita (6) kutoka kwa mwingine.

Hatua kubwa ya kuchukua kupunguza kasi ya kuenea kwa COVID-19 ni kupunguza kugusana kadri iwezekanavyo.

## Nitaenda vipi dukani kwa njia salama?



Nenda wakati haijajaa.

Futa kwa viuavijidudu sehemu ya kushika ya mkokoteni wa dukani.

Usiguse uso wako na mikono yako wakati uko dukani.



Kaa umbali wa futi 6 na watu wengine wakati uko dukani.

Nawa mikono yako ukifika nyumbani.

### Sources:

WHO - <https://www.who.int/emergencies/diseases/novel-coronavirus-2019>

CDC - <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-nCoV/index.html>